

# BARAZA LA FAMASI



## UTARATIBU WA KUHUISHA VIBALI VYA FAMASI KWA MFUMO WA KILEKTRONIKI

### UTANGULIZI

1. **DHUMUNI:** Kutekeleza takwa la Kifungu Na. 36 cha Sheria ya Famasi, Sura 311 (*The Pharmacy Act, Cap 311*).
2. **WAHUSIKA:**
  - Wafamasia wasimamizi wa famasi husika; na
  - Fundi Dawa Sanifu.
3. **MFUMO WA UHUISHAJI:** Mfumo wa Kielektroniki utakaomwezesha Mfamasia Msimamizi au Fundi Dawa Sanifu kuhisha taarifa na kibali cha jengo husika analosimamia kwa mwaka wa fedha 2021/22. Mfumo unapatikana kwa kubofya kiunganishi hapa chini <https://www.pc.go.tz/applications/permitapplication.php>

### LENGO

Kuboresha ufanisi wa uhuishaji wa vibali na uwasilishaji wa taarifa kutoka kwa wasimamizi. Aidha, mfumo utaokoa muda wa uhuishaji na upatikanaji wa vibali husika.

## UTARATIBU WA KUHUISHA KIBALI CHA KUTOA HUDUMA YA DAWA KWENYE REJESTA

- a) **FOMU YA KIELEKTRONIKI:** Mfamasia ANAYESIMAMIA FAMASI au Fundi Dawa Sanifu anayesimamia ADDO YA JUMLA (ARW) atapashwa kuingia katika akaunti yake aliyofungua awali kwenye kanzidata (*database*) ya Baraza.
- b) **Mhuishaji** atapashwa kubonyeza kitufe cha kuhisha na kujaza taarifa zinazohitajika.
- c) **VIAMBATA: Hakikisha kuwa** nakala zote zinazopashwa kuambatishwa zipo katika Mfumo wa PDF. Nakala za kuambatisha ni kama zifuatazo;
  - *A current signed contract of agreement of superintendent pharmacist (period of one year);*
  - **A declaration form if the owner is also a superintendent;**
  - *A current signed commitment form available in the [www.pc.go.tz](http://www.pc.go.tz) (instead of commitment letter) of enrolled/enlisted or dispenser;*
  - *Memorandum of Understanding (pages that show Directors, identification cards recognized by government for personal identification and their signatures);*
  - *Tax Identification Number (TIN) Certificate;*
  - *Business Name Registration Certificate from BRELA;*
- d) Taarifa zote zitakazokuwa zimewasilishwa na mfamasia msimamizi endapo zitakuwa si halali, mfamasia husika atachukuliwa hatua za kisheria.
- e) Baada ya kukamilisha ujazaji wa taarifa, mfumo utakupatia NAMBA YA MALIPO (*Control Number*) ya kulipia kibali ambayo itatumwa kwenye namba ya simu uliyoiingiza.
- f) **KUKAMILISHA UHAKIKI:**

Baada ya uwasilishaji wa taarifa za uhuishaji, uhakiki utafanyika na utakapokamilika utapokea ujumbe wa sms wa kukujulisha upatikanaji wa kibali husika.

Mfamasia/Fundi Dawa Sanifu atawajibika kurudi kwenye akaunti yake kwa ajili ya kudurufu (*printing*) kibali cha duka husika.

- g) **ADA:** Malipo ya ada ya kuhuisha kibali cha biashara kwa mujibu wa Kanuni za Ada na Tozo ya Mwaka 2012 ni kama ifuatavyo:-

Na.	Aina ya Biashara	Ada ya Kibali	Ada ya Taaluma	Jumla
1.	Rejareja	TZS 200,000/=	TZS 200,000/=	TZS 400,000/=
2.	Jumla	TZS 350,000/=	TZS 500,000/=	TZS 850,000/=
3.	Jumla na Rejareja	TZS 550,000/=	TZS 700,000/=	TZS 1,250,000/=
4.	Ghala	TZS 100,000/=	NIL	TZS 100,000/=
5.	Duka la Jumla la ADDO	TZS 200,000/=	TZS 200,000/=	TZS 400,000/=

- h) **MUDA WA MALIPO:** Mfumo utanza kutumika rasmi tarehe **01 Julai 2021** kwa kipindi cha siku 60 ambapo baada ya tarehe **30 Agosti 2021** utalazimika kulipa pamoja na faini ya 25% ya kiwango utakachopaswa kulipia.

**NAMBA ZA SIMU KWA MSAADA:**

Na	Ofisi za Baraza la Famasi	Namba ya simu
1.	Kanda ya kati na magharibi ( <u>Dodoma</u> · <u>Singida</u> · <u>Tabora</u> · <u>Kigoma</u> · <u>Iringa</u> )	0736 222 527
2.	Kanda ya Mashariki ( <u>Dar es Salaam</u> · <u>Lindi</u> · <u>Morogoro</u> · <u>Mtwara</u> · <u>Pwani</u> )	0736 222 523
3.	Kanda ya nyanda za juu kaskazini ( <u>Arusha</u> · <u>Kilimanjaro</u> · <u>Manyara</u> · <u>Tanga</u> )	0736 222 531
4	Kanda ya nyanda za juu kusini ( <u>Mbeya</u> · <u>Njombe</u> · <u>Rukwa</u> · <u>Ruvuma</u> · <u>Songwe</u> · <u>Katavi</u> )	0736 222 521
5	Kanda ya ziwa ( <u>Geita</u> · <u>Kagera</u> · <u>Mara</u> · <u>Mwanza</u> · <u>Shinyanga</u> · <u>Simiyu</u> )	0736 222 528
7.	Makao makuu, Dodoma	0736 222 516

**Imetolewa na:**  
**Msajili,**  
**Baraza la Famasi**  
**S.L.P. 1277,**  
**Bila malipo 0800110015**  
**Dodoma**